FUNZO LA 17

1. Je, nini kilichofanyika wakati wana wa kizazi cha Sethi kilipooa binti wa kizazi cha Kaini?
-Watu wengi zaidi hawakutaka kumsikiliza Mungu.
-Watu wengi zaidi walimsikiliza Shetani pekee.

2. Mungu alisema kuwa angenena na hao watu kwa miaka 120 pekee, je, kama hao watu wangekataa kumsikiliza Mungu, Mungu angefanya nini?
-Mungu angewaadhibu wote kwa kifo.

3. Je, Mungu alikuwa akinena vipi na watu?
-Mungu Roho Mtakatifu alikuwa akinena na hao watu katika akili zao.

4. Je, Roho Mtakatifu alikuwa akiwaambia nini watu?
-Mungu Roho Mtakatifu alikuwa akiwaambia watu wamsikilize Mungu wala sio Shetani.
-Mungu Roho Mtakatifu pia alikuwa akiwaambia watu wafuate njia ya Mungu wala sio njia zao wenyewe.

5. Je, watu wa wakati wa Nuhu walikuwaje?
-Walikuwa wabinafsi.
-Walikuwa wenye dhuluma.
-Hawakutaka njia ya Mungu.
-Walitaka tu njia yao.

6. Je, Mungu aliona dhambi za watu?
-Ndiyo, Mungu aliona dhambi zao zote.



7. Kwa sababu dunia ilijawa na dhambi za watu, Mungu aliamua kufanya nini??
-Kuharibu vyote vyenye uhai duniani.

8. Je, kwa nini Mungu aliamua kumuhifadhi Nuhu?
-Kwa sababu Nuhu hakumsikiliza Shetani.
-Kwa sababu Nuhu alimsikiliza Mungu.
-Kwa sababu Nuhu hakufuata njia yake mwenyewe.
-Kwa sababu Nuhu alifuata njia ya Mungu pekee.
-Kwa sababu Nuhu alijua kuwa Mungu angetuma Mwokozi.

9. Je, Mungu alimwamuru Nuhu kufanya nini?
-Mungu alimwamuru Nuhu kujenga safina.

10. Je, Mungu alitaka Nuhu ajenge safina kwa njia ya Nuhu?
-La.

11. Je, Mungu alitaka Nuhu ajenge aje safina?
-Kama vile Mungu alivyoamuru.

12. Je, Mungu alimwamuru Nuhu kujenga safina ngapi?
-Moja tu.

13. Je, Mungu alimwamuru Nuhu kujenga milango mingapi katika safina?
-Mmoja tu.

14. Ingawaje Nuhu hakuwa amewai kuona mvua awali, Nuhu aliamini nini?
-Kuwa Mungu angetuma gharika.

15. Je, Nuhu alifanya nini alipokuwa akijenga safina?
-Nuhu alipokuwa akijenga safina, aliwaambia watu wamsikilize Mungu.

-Mungu alimwambia Nuhu kuwa alipanga kuleta gharika ili kuwaangamiza watu wote wasiomwamini Mungu.

-Je, Mungu husahau kufanya kile alipanga kufanya?
-La.

-Je, Mungu hufanya kile alisema atafanya?
-Ndiyo.

-Ufuatao ni mfano:

-Siku moja, mtoto wako avunje chungu chako.

-Umkasirikie mtoto wako sana.
-Umwambie mtoto wako kuwa utamwadhibu baadaye.

-Baadaye, usahau kumwadhibu mtoto wako.
-Baadaye, usahau pia kuwa mtoto wako alivunja chungu chako.

-Lakini Mungu si kama watu.
-Watu husahau, lakini Mungu hasahau.

-Mungu alimwambia Adamu kuwa atakufa iwapo angekula lile tunda.

-Je, Adamu alikufa alipokula lile tunda?



-Ndiyo.

-Je, Mungu alisahau alichomwambia Adamu?
-La.

-Je, Mungu alifanya alichosema atafanya?
-Ndiyo.

-Mungu aliwaondoa Adamu na Hawa katika Bustani ya Edeni.

-Mungu si kama watu.

-Mungu hasahau kufanya alichosema atafanya.
-Mungu hufanya anachosema atafanya.

-Mungu hasahau kuhusu dhambi.
-Mungu hasahau kuwadhibu dhambi.

-Mungu huadhibu kila dhambi.
-Mungu huadhibu kila dhambi na kifo.

-Mungu aliwasubiri watu wamwamini yeye.

-Je, Mungu alisubiri kwa muda gani ili watu wa wakati wa Nuhu wamwamini?
-Miaka 120.

-Je, Mungu alipokuwa akiwasubiri watu wamwamini, hasira zake kwa dhambi zao zilipunguka?
-La.

-Mungu alipokuwa akiwasubiri watu wamwamini, hasira yake kwa dhambi zao iliongezeka.

-Hasira ya Mungu kwa dhambi huongezeka tu.

-Hasira ya Mungu kwa dhambi huongezeka hadi wakati ambapo Mungu ataadhibu dhambi.

-Mungu alimwambia nini Nuhu alipomaliza kujenga safina?

Tusome Mwanzo 7:1-4

1-Bwana akamwambia Nuhu, Ingia wewe na jamaa yako yote katika safina; kwa maana nimekuona wewe u mwenye haki mbele zangu katika kizazi hiki.
2-Katika wanyama wote walio safi ujitwalie saba saba, mume na mke; na katika wanyama wasio safi wawili wawili, mume na mke.
3-Tena katika ndege wa angani saba saba, mume na mke; ili kuhifadhi hai mbegu juu ya uso wa nchi yote.
4-Kwa maana baada ya siku saba nitainyeshea dunia mvua, siku arobaini mchana na usiku; na kila kilicho hai nilichokifanya juu ya uso wa nchi nitakifutilia mbali.

-Mungu alimwambia Nuhu afanye nini alipomaliza kujenga safina?

-Mungu alimwambia Nuhu achukue jamii yake na waingie katika safina.



-Mungu alimwambia Nuhu pia achukue wanyama ndani ya safina.

-Wakati wa Mungu kuwaharibu watu ulikuwa umefika.

-Je, kwa nini Mungu alielekea kuwaangamiza watu?

-Watu hawakuamini kuwa walikuwa wenye dhambi.
-Watu hawakuamini kuwa dhambi zao zilistahili kifo cha milele.

-Watu hawakuamini kuwa ni Mungu pekee ambaye angewaokoa.

-Watu hawakuamini ahadi ya Mungu kuwa angetuma mwokozi.

-Mungu alisubiri miaka 120 ili watu waziache njia zao na wafuate njia ya Mungu.

-Lakini watu walitaka tu njia zao.
-Mungu alisubiri miaka 120.

-Mungu hangesubiri zaidi.
-Ulikuwa ni wakati wa Mungu kuwaadhibu watu.

-Leo, Mungu ni yule yule.

-Mungu anawasubiri watu waache njia zao na wafuate njia ya Mungu.

-Siku moja, Mungu hatangoja tena.
-Siku moja, Mungu atawaadhibu watu wote.

Tusome Mwanzo 7:7-11

7-Nuhu akaingia katika safina, yeye, na wanawe, na mkewe, na wake za wanawe pamoja naye; kwa sababu ya maji ya gharika.
8-Na katika wanyama walio safi, na wanyama wasio safi, na ndege, navyo vyote vitambaavyo juu ya nchi,
9-wakaingia katika safina alimo Nuhu, wawili wawili, mume na mke, kama vile Mungu alivyomwamuru Nuhu.
10-Ikawa baada ya siku hizo saba, maji ya gharika yakawa juu ya nchi.
11-Katika mwaka wa mia sita wa maisha ya Nuhu, mwezi wa pili, siku ya kumi na saba ya mwezi, siku ile chemchemi zote za vilindi vikuu zilibubujika kwa nguvu, madirisha ya mbinguni yakafunguka.

-Je, Nuhu na jamii yake waliingia vipi kwenye safina?
-Kupitia kwa mlango wa pekee.

-Je, wanyama wote waliingia vipi katika safina?
-Kupitia kwa mlango wa pekee.

-Huo ndiyo uliokuwa mlango pekee wa kuokolewa.
-Huo ndiyo uliokuwa mlango pekee wa kuepuka adhabu ya Mungu.

-Je, Mungu alimwokoa Nuhu kwa sababu Nuhu alikuwa mzuri?



-La.

-Mungu alimwokoa Nuhu kwa sababu Nuhu alijua kuwa alikuwa ametenda dhambi.

-Mungu alimwokoa Nuhu kwa sababu Nuhu alijua kuwa dhambi yake ilistahili kifo cha milele.

-Mungu alimwokoa Nuhu kwa sababu Nuhu alijua kuwa ni Mungu pekee ambaye angemwokoa.

-Mungu alimwokoa Nuhu kwa sababu Nuhu aliamini ahadi ya Mungu kuwa angemtuma mwokozi.

-Je, ni nini kilichofanyika baada ya Nuhu, jamii yake na wanyama kuingia katika safina?

Tusome Mwanzo 7:16b

16-Bwana akamfungia.

-Baada ya Nuhu, jamii yake na wanyama kuingia katika safina, Je, ni nini kilichofanyika?

-Mungu alifunga mlango.

-Kwa nini Mungu alifunga mlango?

-Ili walio ndani wawe salama.
-Ili walio nje wafe.

-Je, kama watu walio nje wangelia, Nuhu angeweza kuwafungulia mlango?
-La
-Mbona?

-Kwa sababu Mungu alifunga mlango.

-Wakati Mungu alipowaondoa Adamu na Hawa katika Bustani ya Edeni, waliweza kurudi tena?
-La.
-Mbona?

-Kwa sababu Mungu aliwafungia nje ya bustani kwa kuweka malaika na upanga wa moto katika mlango wa bustani.

-Je, yeyote aweza kuepuka adhabu ya Mungu?
-La.

-Mungu anapoamua kuwaadhibu watu, hakuna anayeweza kuepuka.

-Baada ya Mungu kuufunga mlango wa safina, alituma mvua.

Tusome Mwanzo 7:17-20

17-Ile gharika ilikuwako juu ya nchi siku arobaini; nayo maji yakazidi, yakaieleza safina, ikaelea juu ya nchi.
18-Maji yakapata nguvu, yakazidi sana juu ya nchi; na ile safina ikaelea juu ya uso wa maji.
19-Maji yakapata nguvu sana sana juu ya nchi; na milima mirefu yote iliyokuwako chini ya mbingu ikafunikizwa.
20-Maji yakapata nguvu, hata ikafunikwa milima kiasi cha mikono kumi na mitano.



-Je, Mungu aliwezaje kufanya mafuriko yafunika ardhi yote?

-Hapo mwanzo, Mungu alitenganisha Maji.

-Mungu alibakisha maji katika ardhi, na akaweka maji mengine katika anga.

-Ili kufanya mafuriko yafunike ardhi yote, Ili kufanya mafuriko yafunike ardhi yote, Mungu aliyafanya maji yote yaliyokuwa katika anga kunyesha chini.

-Je, watu walikuwa wameona mvua awali?
-La.

-Ijapokuwa watu hawakuwa wameona mvua awali, Mungu alifanya inyeshe siku arubaini.

-Ardhi yote ilifunikwa na maji.
-Hata milima ya juu zaidi na miti mirefu zaidi ilifunikwa na maji.

-Mungu anaweza fanya chochote.
-Hakuna linalomshinda Mungu.
-Ni Mungu pekee mwenye nguvu zote.

-Je, nini kiliwafikia watu wote waliokuwa nje ya mashua?

Tusome Mwanzo 7:21-23

21-Wakafa wote wenye mwili waendao juu ya nchi, na ndege, na wanyama wa kufugwa, na kila mnyama wa mwitu, na kila kitambaacho chenye kutambaa juu ya nchi, na kila mwanadamu;

22-kila kitu chenye pumzi ya roho ya uhai puani mwake kikafa, kila kilichokuwako katika nchi kavu.

23-Kila kilicho hai juu ya uso wa nchi kikafutiliwa mbali tangu mwanadamu hata mnyama wa kufugwa, na kitambaacho, na ndege wa angani; vilifutiliwa mbali katika nchi, akabaki Nuhu tu, na hao walio pamoja naye katika safina.

-Je, nini kiliwafanyikia wanyama wote nje ya safina?
-Walikufa wote.

-Je, nini kiliwafanyikia watu wote waliokuwa nje ya safina?
-Walikufa wote.

-Watu wengi wakati huu hawaamini kuwa wao ni wenye dhambi.

-Watu wenge wakati huu hawaamini kuwa dhambi zao zinastahili kifo cha milele.

-Watu wengi leo hawaamini kuwa ni Mungu pekee anayeweza kuwaokoa.

-Watu wengi leo hawaamini ahadi ya Mungu kumtuma mwokozi.



-Watu wengi leo wanamskiliza Shetani wala si Mungu.
-Watu wengi leo wanapenda dhambi zao.

-Je, wewe ni kama watu wengine au ni kama Nuhu?

-Je, kuna yeyote aliyekuwa nje ya safina aliyeokoka?
-La.

-Mungu alisema kuwa watu wote nje ya safina wangekufa.
-Mungu hufanya kile ameahidi kufanya.

-Je, Mungu alifanya nini baada ya watu wote nje ya safina kufa?

Tusome Mwanzo 8:1-4 & 14-19

1-Na Mungu akamkumbuka Nuhu, na kila kilicho hai, na wanyama wote waliokuwamo pamoja naye katika safina; Mungu akavumisha upepo juu ya nchi, maji yakapungua;

2-chemchemi za vilindi zikafungwa, pia na madirisha ya mbinguni, mvua kutoka mbinguni ikazuiliwa;

3-maji yakadumu kuondoka katika nchi; na mwisho wa siku mia na hamsini maji yakapunguka.

4-Mwezi wa saba, siku ya kumi na saba ya mwezi, safina ikatua juu ya milima ya Ararati.

14-Na mwezi wa pili, siku ya ishirini na saba ya mwezi, nchi ilikuwa kavu.

15-Mungu akamwambia Nuhu, akisema,

16-Toka katika safina, wewe, na mkeo, na wanao, na wake za wanao pamoja nawe.

17-Utoe pamoja nawe kila kilicho hai kilichomo pamoja nawe, chenye mwili, ndege, na mnyama, na kila kitambaacho, chenye kutambaa juu ya nchi; wajae katika nchi, wawe na uzazi, wakaongezeke katika nchi.

18-Basi Nuhu akatoka, yeye, na wanawe, na mkewe, na wake za wanawe pamoja naye;

19-kila mnyama, na kila kitambaacho, na kila ndege, kila kinachokwenda juu ya nchi kwa kabila zao, wakatoka katika safina.

-Mungu alimkumbuka Nuhu na jamii yake katika safina.
-Mungu alisitisha mvua, na akatuma upepo ukakausha ardhi.

-Kuna watu wanaoamini kuwa mapepo wanatawala upepo na mvua.
-Huo ni uongo.

-Ni Mungu pekee aliyefanya upepo na mvua.
-Ni Mungu pekee anayetawala upepo na mvua.

-Mungu aliwalinda Nuhu na jamii yake katika safina.
-Mungu alilinda wanyama wote katika safina.

-Je, kuna yeyote katika safina aliyekufa?
-La.

-Mungu alisema kuwa atawaokoa Nuhu na jamii yake.
-Mungu hufanya kile alichoahidi kufanya.

-Je, Nuhu alifanya nini baada kutoka kwenye safina?



Tusome Mwanzo 8:20-22

20-Nuhu akamjengea Bwana madhabahu; akatwaa katika kila mnyama aliye safi, na katika kila ndege aliye safi, akavitoa sadaka za kuteketezwa juu ya madhabahu.

21-Bwana akasikia harufu ya kumridhisha; Bwana akasema moyoni, Sitailaani nchi tena baada ya hayo kwa sababu ya wanadamu, maana mawazo ya moyo wa mwanadamu ni mabaya tangu ujana wake; wala sitapiga tena baada ya hayo kila kilicho hai kama nilivyofanya.

22-Muda nchi idumupo, majira ya kupanda, na mavuno, wakati wa baridi na wakati wa hari, wakati wa kaskazi na wakati wa kusi, mchana na usiku, havitakoma.

-Kwa sababu Nuhu alifurahi sana  Mungu alipomwokoa, Nuhu alimtolea Mungu dhabihu.

-Je, kwa nini Mungu alikubali dhabihu ya Nuhu?

-Kwa sababu Nuhu alimwamini Mungu.

-Kwa sababu Nuhu aliacha kufuata njia yake na akafuata njia ya Mungu.

-Je, damu ya wanyama ililipa dhambi ya Nuhu?
-La.

-Damu ilimfundisha Nuhu kuwa adhabu ya dhambi ni kifo cha milele.

-Je, Mungu alifanya nini baada ya Nuhu kumtolea dhabihu?

Tusome Mwanzo 9:1-3

1-Mungu akambariki Nuhu na wanawe, akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi.
2-Kila mnyama wa katika nchi atawaogopa ninyi na kuwahofu, na kila ndege wa angani: pamoja na vitu vyote vilivyojaa katika ardhi, na samaki wote wa baharini; vimetiwa mikononi mwenu.
3-Kila kiendacho kilicho hai kitakuwa chakula chenu, kama nilivyowapa mboga za majani, kadhalika nawapeni hivi vyote.

-Mungu alimbariki Nuhu na jamii yake.
-Mungu alimfanya Nuhu kuwa mtawala wa wanyama, ndege na samaki.

-Mungu alimpa Nuhu ishara.

Tusome Mwanazo 9:8 & 11-13

8-Mungu akamwambia Nuhu, na wanawe pamoja naye, akisema,
11-Na agano langu nitalithibitisha nanyi; wala kila chenye mwili hakitafutwa tena kwa maji ya gharika; wala hakutakuwa tena gharika, baada ya hayo, kuiharibu nchi.
12-Mungu akasema, Hii ndiyo ishara ya agano nifanyalo kati yangu na ninyi, na kila kiumbe hai kilichoko pamoja nanyi, kwa vizazi vyote hata milele;



13-Mimi nauweka upinde wangu winguni, nao utakuwa ni ishara ya agano kati yangu na nchi.

-Je, ni ishara ipi ambayo Mungu alimpa Nuhu na watu wote?
-Upinde wa mvua.

-Je, ishara ya upinde wa mvua inamaanisha nini?

-Upinde wa mvua unamaanisha kuwa Mungu hataiharibu dunia tena na mafuriko.

-Je, Mungu ametimiza ahadi yake ya kutoiharibu dunia kwa mafuriko?
-Ndiyo.

-Tangu wakati wa Nuhu, Mungu hajaiharibu dunia na vyote vilivyomo kwa mafuriko.

Tusome Mwanzo 9:18-19

18-Wana wa Nuhu waliotoka katika safina, ni Shemu, na Hamu, na Yafethi; na Hamu ndiye baba wa Kanaani.
19-Hawa watatu walikuwa wana wa Nuhu na kwa hao nchi yote ikaenea watu.

-Je, wana wa Nuhu ambao ni baba wa watu wote ulimwenguni ni nani?

-Shemu, Hamu, na Yafethi.